**WAFILIPI**
**MTAALA**

I. **MAELEZO KWA UJUMLA**.
- A. Mwalimu: Jim Dearman
- B. Mtafsiri: Chris Mwakabanje
- C. Kila darasa linachukua dakika takribani 38.

II. **MAELEZO NA MALENGO**.
- A. Kujifunza kwa kina kitabu cha Wafilipi na kusisitiza "nia ya Kristo," ambayo ndio ufunguo wa kuridhika na kuzidi kufurahi "katika Bwana."
- B. Mwanafunzi atatiwa nguvu kwa kujifunza na kutumia kanuni ambazo Paulo anafundisha katika waraka huu.
- C. Mwanafunzi ataelewa ni mambo gani kanisa linapaswa kufanya ili limpendeze Bwana.
- D. Mwanafunzi ataweza kufundisha wengine ukweli kutoka katika kitabu hiki kwa wengine.

III. **VIFAA VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA KUJIFUNZA**.
- A. Unapaswa uwe na vifaa vifuatavyo:
  1. Biblia (Swahili – UV, English – ASV, KJV, NKJV).
  2. Masomo kwa video yote.
  3. Maelezo (Notes) ya kozi hii yote.

- B. Maoni: Tunapendekeza uwe na hotuba kutoka katika Wafilipi, na Tom Holland, Reason To Rejoice, (Holland Publication, 1975).

- C. Kitabu chochote cha fafanuzi (commentary) kinachoshikilia mafundisho ya awali katika Wafilipi.

IV. **MAMBO YA KUFANYA KATIKA KOZI HII**:
- A. Usome kitabu chote cha Wafilipi angalau mara tano.
- B. Angalia kikamilifu kanda za video zote.
- C. Usome kikamilifu notisi zote za darasani.
- D. Kamilisha kazi yote ya kudondoa (maelezo hapo chini).
- E. Wasilisha makala ya muhula (maelezo hapo chini).
- F. Hakikisha unafanya mtihani mmoja.
- G. Unapaswa ufaulu kwa kiwango cha angalau asilimia 70.

V. **KAZI YA KUDONDOA**.
- A. Mistari ya kudodoa lazima iandikwe (au ichapwe) bila kutazamia mahali, kisha itumwe VBI kwa masahihisho. Mistari ni lazima itoke katika UV kama ulivyoonyeshwa katika fomu yako ya maombi ya kujiunga na VBI.

- B. Mistari yote ni sharti iandikwe ama kuchapwa katika mkao mmoja (mara moja). Unaweza kujifunza zaidi na kuianza upya yote iwapo ulikosea, lakini unapaswa kuanza upya yote na kuiandikwa katika mkao mmoja.

- C. Kwa kozi hii, mistari ifuatayo inapaswa kudondolewa:
  Wafilipi 1:9-11 Wafilipi 2:5-8 Wafilipi 3:13-14
  Wafilipi 4:6-8 Wafilipi 4:13

D. Kazi ya kudondoa uiwasilishe VBI wakati unatuma mtihani wako wa tatu.
E. Maoni: Njia bora ya kudondoa ni kuandika mistari katika vijikadi ili kwamba iwe rahisi kwako kuipitia mara kwa mara muda wote unavyoendelea na kozi hii.

**VI. MITIHANI.**

A. Kuna mtihani mmoja wa kufanya katika Wafilipi.

B. Unapokaribia mwisho wa kitabu, wasiliana nasi na kuomba mtihani.

C. Ukishapokea mtihani, unaruhusiwa kuupitia na kujifunza.

D. Walakini, unapofanya mtihani, unatakiwa uufanye wote bila kutazamia katika notisi, Biblia, kitabu, n.k.

**VII. MAKALA YA MUHULA.**

A. Andika makala juu ya muhtasari wa Wafilipi ukielezea mambo muhimu katika kila sura na kutoa masomo ambayo tunaweza kujifunza.

B. Makala inapaswa kuwa na kurasa angalau nne za kuchapwa ukiacha nafasi mbili-mbili (double spaced). Kama umeandika kwa mkono, makala isipungue kurasa sita bila kuruka msitari (single spaced).

C. Makala itatakiwa unapotuma mtihani wako wa mwisho VBI pamoja na dondoa.

**VIII. MAKSI.**

A. Kazi ya kudondoa, makala ya muhula, na mtihani zitasahihishwa tofauti tofauti.
B. Maksi za mwisho zitazingatia juu ya wastani wa kazi zako zote ulizopewa.
C. Unaweza kuomba fafanuzi na kufikiriwa juu ya maksi, lakini kwa vyovyote vile VBI ndiyo yenye uamuzi wa mwisho.

IX. **TUNZO**.

A. Tunzo itatolewa, ikiwa ni pamoja na cheti, pale tu utakapokuwa umefanikiwa kumaliza kazi zako kikamilifu, umerejeza kanda za video (kama uliziazima), na ada yote kwa kozi hii umelipia.

B. Mungu na abariki jitihada yako ya kujifunza neno lake lenye uvuvio!

## UTANGULIZI

Mji wa Filipi ulikuwa moja ya miji mikubwa ya Makedonia (Mdo.16:12). Ulipatikana Kaskazini mwa Uyunani karibu na pwani ya bahari, takribani maili 8 au 10 kutoka bandari ya Nikapoli. Mji huu ulikuwa katika barabara iliyotoka Ulaya kuelekea Asia, na hata kuumfanya mji kuwa muhimu kwa injili. Kwa ujumla Paulo alichagua eneo hilo kuwa mahali pa kuanzia kazi zake.

Filipi wa Makedonia, ndiye alikuwa babaye Alexander Mkuu, ambaye alikalia kiti mwaka 360 K.K., akautwaa mji wa Krenides, akaanzisha koloni ndani ya mji, na kuuita mji kwa jina lake. Jimbo la Makedonia baadaye lilitwaliwa na Warumi na kugawanywa katika wilaya nne. Vita vya Filipi katika mwaka 42 K.K. ndivyo vilivyotoa mshindi katika historia. Hapo katika Filipi, Mark Antony na Octavian walimshinda Brutus na Cassius na kutoa nafasi kwa ufalme wa Rumi.

Baada ya mji wa Filipi kuwa chini ya koloni la Rumi, lugha ya watu ikawa Kilatini, kadhalika fedha, sheria, na utamaduni wa Kirumi ulishamiri zaidi (Mdo.16:20,21). Mji ukastawi chini ya utawala wa Rumi. Wayahudi wachache tu ndio waliishi katika mji huu, na hapakuwa na sinagogi katika mji huo (Mdo.16:13). Kulikuwa na shule ya utabibu katika mji huu, jambo ambalo ni la kuvutia, kwa kuwa Luka tabibu aliishi katika mji huu. Leo hii pamekuwa na mabaki tu ya mji.

Paulo awali kabisa alifika katika mji huu 52 B.K. katika safari yake ya pili ya umisionari. Matendo 16 hutoa taarifa za kutembelea kwake. Ni mji wa kwanza Paulo kuhubiri injili Ulaya. Katika safari yake ya tatu ya umisionari, Paulo alitembelea tena Filipi, kadhalika katika makanisa mengine ya Makedonia. Safari hii ilikuwa baada ya miaka mitano ya safari ya kwanza. Inaonekana kuwa palikuwa na urafiki wa karibu sana na upendo wa dhati baina ya Paulo na kanisa hili kuliko makusanyiko mengine yoyote. Kusanyiko hili lilimsaidia Paulo kifedha mara nyingi (Flp.4:15,16; 2 Kor.11:9). Makanisa ya Makedonia yalijulikana kwa ukarimu (liberality) – 2 Kor.8:1-5. Ingawa walikuwa maskini kuliko wengine wengi, walakini walikuwa wakarimu sana.

## MUHTASARI KWA UFUPI WA WAFILIPI

1. Salaam ………………………………………………… 1:1,2
2. Shukrani na sala kwa ajili ya Wafilipi ………………… 1:3-11
3. Kuenea kwa injili katika Rumi …………………………… 1:12-18
4. Matarajio ya Paulo …………………………………………. 1:19-26
5. Anasihi kuishi maisha bora yanayostahili ………………….. 1:17-2:18
6. Sisitizo juu ya kufuata kilelezo cha Kristo ………………. 2:5-11
7. Habari kuhusu Timotheo na Epafradito …………………… 2:19-30
8. Waalimu wa uongo dhidi ya mfano wa Paulo ………………… 3:1-4:1
9. Anasihi juu ya kila mtu kuishi kwa amani ……………….. 4:2,3
10. Anasihi kuhusu furaha ………………………………………. 4:4-7
11. Anasihi juu ya kutafakari mambo mema ……………………… 4:8,9
12. Anawashukuru kwa ajili ya zawadi zao ……………………. 4:10-20
13. Salaam ……………………………………………………… 4:21-23

## NDANI YA KITABU KUNA MSINGI WA UMOJA

1. Wafilipi 1 hukazia jinsi (attitude) ya kushukuru.
   a. Kwa ajili ya ushirikiano (1:3-11).
   b. Kwa ajili ya ushindi (1:12-18).
   c. Kwa ajili ya wokovu (1:19-26).

2. Wafilipi 2 hujadili nia (mind or attitude) ya Kristo.
   a. Wakristo wanapaswa kuwa na nia aliyokuwa nayo Kristo.
   b. Timotheo alisifiwa kwa kuwa na nia ya Kristo (2:19-21).

3. Wafilipi 3 hukazia jinsi ya kuthamini mambo sahihi.
   a. Paulo alivihesabu vitu vyote kuwa hasara kwa ajili ya Kristo (3:8).
   b. Aliwasihi kuwa na nia kama hiyo (3:15).

4. Wafilipi 4 husisitiza msimamo juu ya mambo mema (virtues) mengi.
   a. Umoja – muwe na nia moja (4:2).
   b. Furaha – furahini katika Bwana (4:4).
   c. Mawazo safi – tafakarini hayo (4:8).
   d. Kuridhika – "nimejifunza kuwa radhi na hali yoyote ile" (4:11).
   e. Shukrani (4:18).

Mtu mmoja ameutaja waraka kwa Wafilipi kuwa ni "Ni waraka wa upendo wa Paulo." Upendo mwingi umedhihirika kwa ndugu hao na sifa nyingi. Walisimama na Paulo na kumsaidia mahitaji yake, n.k. Angalia 4:15,16; 2 Kor.11:9. Paulo hakuwahi kuwalemea watu wa Makedonia, bali alikuwa na shukrani nyingi kutokana na misaada aliyoipokea kutoka katika mikono yao. Angalia pia 2 Kor.8:1-5. Walitoa zaidi ya matarajio ya Paulo. Siri ya utoaji wa jinsi hii – 2 Kor.8:5 – kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana.

Misimamo (attitudes) ni muhimu sana. Kwa sababu ya upendo wao kwa Bwana, walikuwa tayari kujitoa sadaka. Linganisha Musa.

Ndiyo sababu basi Paulo alilipenda na kulifurahia sana kanisa hili.

## SURA YA KWANZA

**UTANGULIZI**

1. Wafilipi sura 1 huelezea jinsi ya kushukuru.
2. Paulo anashukuru kwa ushirikiano na ndugu wa Filipi, ushindi wake katika Kristo, na tumaini la wokovu.

**FAFANUZI**

I. Salaam na kujitambulisha (1:1,2).
   A. Paulo na Timotheo wametajwa kuwa ni watumwa wa Kristo.

   B. Wafilipi wametajwa kuwa ni "watakatifu."
      1. "Mtakatifu" = mtu aliyetengwa kwa matumizi matakatifu.
      2. Wakristo wote ni watakatifu (1 Pet.1:15,16).

   C. Maaskofu na mashemasi wametajwa.
      1. Maaskofu ni wazee, waangalizi (bishops), au mapasta wa kusanyiko.
      2. Majina yote hapo juu yanataja ofisi moja.
      3. Mashemashi ni watumishi maalum wa kanisa, wakifanya kazi chini ya usimamizi wa wazee.
      4. Sifa za wazee zimeorodheshwa katika Tito 1:5-9 na 1 Timotheo 3.
      5. Sifa za mashemasi zimeorodheshwa katika 1 Timotheo 3:8-13.

D. Katika mstari 2, Paulo kama kawaida yake anatoa salaam, pamoja na kuwatakia neema na amani ziwafikie ndugu hao wema.

II. Shukrani za Paulo zimebainishwa na hali aliyokuwa nayo katika Rumi (1:3-30).

A. Kubainishwa sala na shukrani za Paulo katika kanisa la Filipi katika mistari 3-11.

1. Mstari 3 na 4 haswa ni kwa ajili ya kuigwa, na wala si kwa kuelezea tu.

2. Paulo alishukuru kutokana na ushirika wa Wafilipi (mstari 5).
   a. Ushirika ni fungu ambalo mtu anakuwa nalo katika jambo lolote; kushiriki (participation), mwungano (association), au kuwa pamoja (communion).
   b. Neno la Kiyunani "*koinonia*" limetafsiriwa:
      1) "Ushirika" – Film.6 (communication).
      2) "Ushirika" – 1 Kor.10:16 (communion).
      3) "Changizo" – Rum.15:26 (contribution).
      4) "Washirikisha" – 2 Kor.9:13 (distribution).
      5) "Ushirika" – Filp.1:5 (Fellowship).

3. Paulo anaelezea msimamo wake kwamba Wafilipi waumalize mwendo wao, na anatoa sifa muhimu katika kutekeleza hayo (mistari 6-11).
   a. Katika mstari 6, "siku ya Kristo" ni siku ya hukumu.

   b. Paulo anaelezea jinsi alivyomwamini Mungu kwamba angeikamilisha kazi aliyoianza pamoja nao.

   c. Mstari 7 na 8, Paulo anabainisha kwamba ni sahihi kuwaombea kama mtu aliyewapenda na kuwa mshiriki pomaja nao wa neema ya Mungu.

   d. Sifa za Mkristo anayehitaji kukamilisha mwendo wake:
      1) Pendo lake liwe jingi – mstari 9.
      2) Katika hekima – mstari 9.
      3) Ufahamu (KJ – judgement) – mstari 9.

   e. Matokeo ya kuwa na tabia kama hiyo:
      1) Uwezo wa kuyakubali yaliyo mema – mstari 10
      2) Uwezo wa kuwa na mioyo safi (sincere), bila waa – mstari 10.
      3) Kujazwa matendo ya haki – mstari 11.

   f. "Mioyo safi" (sincere) katika mstari 10 haswa ikimaanisha, "kitu ambacho kimetazamwa katika mwanga wa jua na kuonekana safi pasipokuwa na waa."

   g. Angalia kwamba matunda mstari 11 yanapaswa kutazamwa kama matokeo ya kuwa Mkristo, ni kwa ajili ya utukufu na sifa mbele za Mungu, na wala si kwa ajili ya mwanadamu.

B. Msimamo wa Paulo kulingana na hali yake akiwa Rumi imedhihirika katika 1:12-30.

1. Katika mistari 12-18 Paulo anaandika juu ya kuenea kwa injili Rumi.
   a. Paulo aliwataka ndugu wasiwe na wasiwasi juu yake (mstari 12).

   b. Aliwahakikishia kwamba kwa majaliwa ya Mungu aliweza kuhubiri kwa askari kama matokeo ya vifungo vyake (mstari 13).

   c. Linganisha na Wafilipi 4:22, Paulo anaandika kuhusu watu wa nyumbani mwa Kaisari ambao waliongolewa.

   d. Mstari 14 – Paulo akionyesha mfano wa ujasiri aliwasaidia ndugu zake kuwa na ujasiri zaidi katika kuihubiri injili.
      1) Hili hudhihirisha nguvu zitokanazo na ushawishi (influence).
      2) Ni sharti kila Mkristo awe nuru. Linga. Math.5:16.

   e. Mistari 15-18 hujadili nia tofauti-tofauti za wahubiri.
      1) Wengine walimwongezea dhiki Paulo kutokana na mahubiri yenye nia mbaya (insincere).
      2) Hata hivyo, wengine kwa nia njema yenye upendo katika mahubiri yao.
      3) Katika mstari 18 Paulo alifurahi kwamba Kristo alikuwa akihubiriwa hata ingawa wengine hawakuwa na nia njema.
         a) Paulo hasemi kwamba hao wenye nia mbaya walikubaliwa na Mungu, la hasha.
         b) Alifurahia kwamba elimu kuhusu Kristo ilienezwa.
         c) Watu watapotea milele kutokana na nia mbaya. Linga. Yoh.4:24.

2. Tumaini lake Paulo limebainishwa katika 1:19-26.
   a. Paulo alikuwa na imani kubwa akiwaombea ndugu zake.
   b. Aliamini kwamba kupitia sala na Roho wa Kristo, angeshinda kila jaribu. Linga. Filp.4:13.
   c. Leo tunashinda kupitia upanga wa Roho, Neno la Mungu (Efe.6:17).
   d. Paulo anaelezea mtanziko (dilemma) katika mistari hii.
      1) Ni heri nikaondoka na kukaa pamoja na Kristo.
      2) Lakini kwa ajili ya ndugu inanilazimu nibaki nipate kuyaangalia makanisa.
   e. Paulo alitambua kwamba ndugu wangefurahia kumwona mara nyingine
   f. Kwa hiyo, alikuwa na imani katika majaliwa ya Mungu kwamba angetoka jela.
   g. Tafakari juu ya mtu huyu asiye na ubinafsi katika kuwajali wengine wakati yeye mwenyewe akiwa gerezani Rumi!

3. Katika mistari 27-30 Paulo anawatia moyo Wafilipi:
   a. Kusimama imara pamoja – mstari 27.
   b. Kushindania imani pamoja – mstari 27.
   c. Kwa pamoja wasiogope adui – mistari 28-30.
   d. Daima wadumu katika mwenendo (conversation) sawasawa na ipasavyo injili.
   e. Faraka imepingwa siku zote katika Maandiko. Linganisha 1 Kor.1:10-13.
   f. Mateso yalipaswa kutazamwa kama fursa na wala si mzigo.

**HATIMISHO**
1. Sura 1 ya Wafilipi hukazia jinsi ya kushukuru.
2. Neno "Kristo" katika sura hii limetajwa mara 16.

## SURA YA PILI

**UTANGULIZI**:
1. Wafilipi sura 1 hukazia juu ya jinsi ya kushukuru.

2. Wafilipi 2 hukazia nia ya unyenyekevu pamoja na umoja.
3. Nia ya Kristo ni mfano bora ambayo Wakristo wote wanapaswa kuiga (Filp.2:5).

I. Kielelezi cha Bwana kwa kanisa kimewekwa bayana na Paulo (2:1-18).
   A. Mfano wa Kristo umedhihirika, kuanzia unyenyekevu hata kufikia kuinuliwa (2:1-18).
      1. Mistari 1-4 Paulo anawasihi Wafilipi wawe wamoja wakizingatia sababu zifuatazo:
         a. Wako ndani ya Kristo,
         b. Walipaswa kusukumwa na upendo,
         c. Ushirika wao ni kwa maongozi ya Roho Mtakatifu, na
         d. Ukristo unahitaji rehema na utu wema.

      2. Pia tunaona orodha ya matendo ambayo husababisha umoja.
         a. Tuwe na nia (mind) moja.
         b. Wenye mapenzi mamoja.
         c. Wenye roho moja (one accord - kupatana).
         d. Mkinia mamoja, kuungana kifikra.
         e. Tukizuia faraka na majivuno matupu (vainglory).
         f. Wenye unyenyekevu (linga. Rum.12:3).
         g. Bila kuwa wabinafsi kwa wengine (linga. Rum.12:9,10).

      3. Ombi la mwisho na la msingi zaidi juu ya umoja limeonekana katika mistari 5-11, mfano wa Yesu.
         a. Nia (mind) ya Kristo ni msimamo (attitude) wa Kristo.

         b. Ni jinsi gani msimamo ulidhihirika ndani ya Kristo?
            1) Aliacha hali ile ya kuwa sawa na Mungu, akatwaa namna na mfano wa mtumishi (mistari 6,7).
            2) Alijinyenyekeza, akawa ana namna ya mwanadamu na kwa hiari akafa kwa ajili yetu (mst. 8). Linga. Yoh.10:17,18.

         c. Ikiwa ni matokeo ya kujitoa kwake sadaka, Mungu alimwinua, akimrejezeshea utukufu ambao alikuwa nao kabla ya kuja duniani (mistari 9-11). Linga. Yoh.17:5.
            1) Jina alilopewa ni "Bwana," pengine likionyesha mamlaka yake (mst.9).
            2) Na baadaye kila mtu atamkiri (mst.10).
               a) Jeshi la malaika linamwabudu yeye.
               b) Nao hao walio duniani wanamkiri yeye.
               c) Mapepo yanaamini hata na kutetemeka (Yak.2:19).

            3) Kwa kumkiri hivyo Kristo humletea Mungu heshima na utukufu (mst.11).

   B. Mungu anawahamasisha waumini kuenenda kwa utiifu mbele za Kristo hata kufikia utukufu wa mwisho (2:12-18).
      1. Wokovu wa mwanadamu ni juhudi inayohusisha Mungu na mwanadamu.
         a. Mwanadamu anayo majukumu ya kufanya, kazi ya imani (mst.12).
            1) Efe.2:10.
            2) Tito 2:14.

         b. Mungu anatenda kazi pamoja na wamwaminio kupitia neno lake, ambalo hubainisha mapenzi na jinsi ya utendaji.
            1) Neema ya Mungu imekuja ikifundisha.

   2) Lazima tuipokee (respond) neema yake kwa kuitendea kazi kwa hiari. Linga. Tito 2:11-14.

2. Mungu anajali “jinsi gani” tunavyofanya mambo, kadhalika “ni kitu gani” tunachofanya (mst.14).
   a. Kunung’unika ni dhambi nzito sana.
      1) Hesabu 11:1-3.
      2) 1 Kor.10:10.

   b. Kushindana ni dhana ya ubishi wa hadharani ambao hata hufikia hatua ya kunung’unika.

   c. Mambo yote hayo yanakatazwa katika Maandiko.

   d. Hata ingawa mtu hutii, na kisha ananung’unika na kushutumu, huyo hampendezi Mungu.

   e. Je, mtoto anayetii, wakati huo huo ananung’unika, huyo anawapendeza wazazi wake?

3. Matokeo ya kutii kwa nia njema yameonekana katika mstari 15.
   a. “Wasio na lawama” – yaani mtu asiye na shutuma yoyote, au asiyestahili kukaripiwa. Linga. Lk.1:6.
   b. “Wasio na ila” (harmless) – ni wazo la usafi, kukaa mbali na uovu.
   c. Kizazi chetu ni “cha ukaidi na kilichopotoka.”
      1) Tunaweza kugeuza maovu kuwa mema na mema kuyafanya maovu.
      2) Linganisha Isaya 5:20.
   d. Mbali ya haya yote, Mkristo anapaswa kuangaza mithili ya nuru. Linga. Math.5:16.

4. Mstari 16 tunaona kwamba tunapaswa kulipeleka neno la Mungu kwa wengine.
   a. Paulo alielewa kwamba uongofu wake ulikuwa ni kuwaongoa wengine akiwa nuru ya ulimwengu ulio gizani.
   b. 1 Kor.3:11-15 – Hujadili thawabu ya mtu ambaye waongofu wake wamestahimili.

5. Mistari 17 na 18 panataja furaha wakati tupatapo mateso kwa ajili ya Kristo.
   a. Fungu la maneno, “nikimiminwa juu ya madhabahu” haswa ikimaanisha “nikimwagwa madhabahuni kama sadaka ya vinywaji.”

   b. Sadaka ya vinywaji ilikuwa sehemu ya mpango wa Agano la Kale (linga. Hes.15:4,5).

   c. Paulo anafananisha utumishi na sadaka za Wafilipi kuwa ni dhabihu ya kuteketezwa, na akalinganisha maisha yake kuwa sadaka ya vinywaji vilivyomiminwa kuwa dhabihu kama mchango kwa uaminifu wake.

   d. Maisha ya Paulo yanaweza kufikia hatima Rumi, lakini anawasihi Wafilipi wafurahi pamoja naye kwa fursa hiyo ya kuteseka kwa ajili ya Kristo.

II. Paulo anawataja watenda kazi pamoja naye katika injili (2:19-30).

A. Timotheo ametajwa katika mistari 19-24.

1. Paulo alimwamini Timotheo kiasi kikubwa na mara nyingi alimtuma kwa makanisa ambayo yalihitaji msaada wa Paulo ambapo Paulo alishindwa kufika.

    a. 1 Thes.3:1,2.
    b. Mdo.19:22.

2. Paulo anaandika katika mstari 21 juu yao watakao faida zao wenyewe, lakini Timotheo ni mtu tofauti.
    a. Wafilipi walikuwa tayari wameuona uaminifu wa Timotheo.
        1) Uaminifu hudhihirika kwa njia ya matendo.
        2) Katika 1 Thes.1:3 Paulo anaandika juu ya "kazi yenu ya imani."
        3) Yakobo anadai kwamba imani isiyo na matendo imekufa (Yak.2:24).

    b. Wakati huo Paulo alikusudia kumtuma Timotheo kwao, lakini alimtumaini Mungu kwamba angemwokoa ili yeye mwenyewe aweze kufika kwao.

3. Katika mistari 25-30 Paulo anamjadili mjoli mwingine mwaaminifu, Epafradito.
    a. Hapa tunaona mtu ambaye alifanya kazi karibu ya kufa kwa ajili ya Kristo.

    b. Angelikuwa amekufa, wasifu (epitaph) wake ungesomeka namna hii:
        1) Ndugu,
        2) Mtenda kazi pamoja nami,
        3) Askari pamoja nami,
        4) Tena ni mtume (messanger) wenu, na
        5) Mhudumu.

    c. Ni sifa kubwa ajabu Paulo alizoziorodhesha kwa ajili ya mtu huyu Epafrodito?

    d. Mtu huyo alitumwa kwa Paulo kama mjumbe, ni mtu ambaye angemsaidia Paulo katika kazi.

    e. Sasa alitaka kurejea Filipi kwa sababu ya ugonjwa.

    f. Epafrodito alijifunza kwamba ndugu zake kule Filipi walijua habari juu ya ugonjwa wake.

    g. Hakutaka wajisumbue juu yake.

    h. Hiyo tabia njema ajabu iliyokuwa ndani ya mtu huyu, iliyo kinyume kabisa na watu wengi kanisani siku zetu hizi ambapo watu hupenda hali zao zitambulikane.

    i. Fungu hili linadhihirisha kwamba Wakristo wanaweza kuugua magonjwa na hata kufa.
        1) Paulo hakumponya kimiujiza Epafrodito.
        2) Miujiza ilitendwa kwa ajili ya kulithibitisha neno.
        3) Paulo alimwacha Trofimo akiwa mgonjwa Mileto (2 Tim.4:20).
        4) Paulo mwenyewe alikuwa na mwiba mwilini mwake (2 Kor.12:7-9).

    j. Paulo alimshukuru Mungu kwa kumponya Epafradito (mst.27).
        1) Kama Epafrodito angelikufa, Paulo angelihuzunika sana.
        2) Paulo aliweza kuona baraka zake daima, hata katika uadui.

    k. Paulo, roho yake isiyo na ubinafsi imeonekana katika maelezo mstari 28.
        1) Paulo angefurahia ikiwa Wafilipi wangeungana na mjumbe.

2) Alijali sana furaha yao kuliko ya kwake.

l. Katika mistari miwili ya mwisho ya sura hii Paulo anawakumbusha Wafilipi kwamba Epafrodito alihatarisha maisha yake akitenda kazi ambayo walimtuma aifanye.

m. Ingawa mtu huyu ametajwa hapa na katika Filp.4:18; walakini ni mtumishi bora ambaye anapaswa kuigwa.

n. Epafrodito ni shujaa mkubwa wa imani.

**HITIMISHO:**
1. Sura hii muhimu inatufundisha umuhimu wa unyenyekevu na kujikana wenyewe katika kuuhifadhi umoja.
2. Watu watatu waliorodheshwa humu, Paulo, Timotheo, na Epafrodito, ni mifano bora katika unyenyekevu.
3. "Heri walio maskini wa roho; maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Math.5:3).

## SURA YA TATU

**UTANGULIZI:**
1. Sura 3 ya Wafilipi hutoa tofauti kati ya waalimu wa uongo na Paulo.
2. Sura hii pia inatupatia jinsi Paulo alivyojitoa sadaka kwa ajili ya injili.
3. Paulo anawasihi Wafilipi kwamba wamfuate yeye kama alivyokuwa akimfuata Kristo (linga. 1 Kor.11:1).

**MAZUNGUMZO:**

I. Roho ya Paulo ni kinyume kabisa na waalimu wa uongo katika 3:1-16.
   A. Jukumu la kufurahi katika Bwana limebainishwa katika mstari 1, kama ilivyo katika mistari mingine ya injili.
      1. Linganisha 2:18 na 4:4.
      2. Maneno haya yanaoonyesha tendo la kudumu –"endelea kufurahia."
      3. Katika mtari huu Paulo pia anawakumbusha wasomaji wake kwamba jambo la kurudia kuandika mambo yale yale halimsumbui.
      4. Kurudia-rudia huko kunawafanya Wakristo wawe imara katika imani (linga. 2 Pet.1:12).

   B. Mstari 2 unaanza na maonyo juu ya waalimu wa Kiyahudi ambao walikuwa wakijaribu kushurutisha sheria za Musa juu ya Wakristo.
      1. Wametajwa kuwa "mbwa" wanyama ambao walikuwa najisi kwa Wayahudi (Math.7:5).
      2. Mataifa waliitwa mbwa (Math.15:26,27).
      3. Waalimu hawa wa uongo walitajwa hivyo kwa kuwa walikuwa wakiigeuza injili, walikuwa wakishurutisha tohara juu ya Wakristo.
      4. Paulo aliwaita "wajikatao" ikimaanisha "kujikata mwili bila faida."
      5. Tohara ilikuwa haina umuhimu (Gal.6:15).

   C. Wakristo ndiyo tohara haswa, watu wa kweli wa Mungu (mst.3).
      1. Rum.2:25-29.

      2. Gal.6:15,16.

3. Kuna alama tatu za tohara ya kweli:
    a. Kuabudu katika Roho wa Mungu.
    b. Kuwa na furaha katika Kristo Yesu, na
    c. Kutoutumani mwili.

4. Kuabudu katika Roho ni ibada sawasawa na sheria ya Agano Jipya iliyotolewa na Roho.

5. Ni ujinga kumtumikia Mungu chini ya Sheria ya Kale leo. Linga. Gal.3:1-3.

D. Paulo anaorodhesha vitu alivyowahi kuviamini kwa mtazamo wa mwili (mistari 4-6).
1. Paulo alikuwa na mambo ya msingi ya kutumainia katika utaratibu wa Kiyahudi kuliko waalimu hao wa Kiyahudi (mst.4).

2. Angalia orodha ya msimamo wa Paulo kama Mwebrania.
    a. Alitahiriwa siku ya nane (linga. Lk.1:59; 2:21).
    b. Ni mtu wa taifa la Israeli (linga. 2 Kor.11:22).
    c. Wa kabila la Benyamini (linga. Rum.11:1).
    d. Paulo alikuwa Farisayo (linga. Mdo.23:6; 26:5).
    e. Mwenye bidii katika kuliudhi kanisa, lakini jitihada yake ilitokana na ujinga na chuki binafsi juu ya Ukristo (linga. Rum.10:1-3).
    f. Paulo alikuwa hana hatia kwa habari ya kuifuata torati.

3. Mambo hayo sita yanaonyesha kuwa Paulo angeweza kupata heshima zaidi, kama alitaka kufanya hivyo, kwa mtazamo wa Kiyahudi kuwazidi waalimu hao wa Kiyahudi.

E. Lini Paulo alihesabu mambo hayo yote yenye heshima na ubora kuwa hasara? (mstari 7).
1. Aliyahesabu kuwa hasara alipofanyika kuwa Mkristo.
2. Angalia mambo aliyoyahesabu kuwa hasara:
    a. Fahari za kimwili na jadi (ancestry) ni hasara,
    b. Nafasi yake miongoni mwa Mafarisayo ni hasara, na
    c. Kufuata desturi ilikuwa hasara kwake.
        1) Alikuwa na haki ipatikanayo na sheria.
        2) Aliheshimiwa na watu wake kama mtu mwenye bidii katika kuishika sheria.

F. Katika mstari 8-11 Paulo anaeleza kwamba anazidi kuyahesabu mambo hayo kuwa hasara ukilinganisha na faida alizopata katika Kristo.
1. Paulo “alihesabu” na angali “anahesabu” kuwa hasara mambo yote ambayo yangezuia huduma yake kwa Kristo.
2. Ni mambo gani aliyapata katika Kristo?
    a. Alipata maarifa yenye uzima wa milele (mstari 8; linga. Yoh.17:3).
    b. Alihesabiwa kuwa na haki kwa njia ya imani (mstari 9; linga. Rum.5:1).
    c. Alipata kushiriki mateso ya Kristo (mstari 10).
    d. Alifanyika kuwa mtume wa Kristo (linga. Mdo.9:15).
    e. Alipata tumaini la kufufuliwa katika uzima wa milele (mstari 11).

G. Nia ya Paulo kuhusu mambo yaliyopita na yajayo imebainishwa katika mistari 12-14.
1. Paulo hakuwahi kusema kwamba hajawahi kutenda dhambi.
2. Lengo lake hasa lilikuwa kuyasahau mambo yaliyopita ambayo yangemzuia asisonge mbele hata kuifikia mede (prize) ya uzima wa milele.

3. Tunapaswa kuviweka pembeni vitu vyote ambavyo vitatuzuia tusikimbie mbio na kupata thawabu la mbinguni (linga. Ebr.12:1,2).
4. Hamasa ya Paulo ya kusonga mbele ili kufikia lengo lake ilitokana na upendo wa Kristo uliodhihirika kwa njia ya msalaba.
   a. Paulo alishurutishwa na msalaba – 2 Kor.5:14,15.
   b. Paulo alilazimishwa na msalaba – Filp.3:13,14.
   c. Paulo aliongozwa na msalaba – Filp.4:1ff.

H. Mistari 15 na 16 ni hitimisho lenye kuonyesha mkazo kwa kuzingatia mistari iliyotangulia.
   1. Paulo anawasihi hao wanaojidhania kuwa ni Wakristo wakomavu kutambua kuwa wanapaswa kuchuchumilia malengo yaliyo mbele yao.
   2. Kuna sheria za kuzifuata – Agano Jipya – linga. Gal.6:16.

I. Mstari 17 huhusisha kwa karibu hoja za mstari 9 katika sura 4.
   1. Wafilipi waonywa kwamba wamfuate Paulo (linga. 1 Kor.11:1).
   2. Paulo aliweka bayana kiolezo (pattern) ambacho aliwaomba wakifuate.
   3. Ni wahubiri wangapi wangeweza wakati wote kufanya hivi?

J. Katika mstari 18 na 19 anaandika watu ambao hawafai kuigwa au kufuatwa.
   1. Paulo hakusita kuwaonya juu ya waalimu wa uongo.
   2. Walakini, angalia msimamo wake.
      a. "Hata kwa machozi" ni jinsi alivyofunua Paulo huruma juu ya roho.
      b. Katika Matendo 20:31 roho hiyo hiyo imeonekana katika maelezo ya Paulo "kwa machozi."
      c. Paulo aliwaonya na kulia, akionyesha kwamba hatupaswi kuridhia kati ya ukweli na uongo, bali tunapaswa kuzihurumia roho zilizo dhambini.
      d. Watu lazima waone ni jinsi gani tunaichukia dhambi, lakini hili lisitufanye kuonyesha dhahiri roho mbaya juu ya watenda dhambi.

K. Katika mistari ya mwisho ya sura hii, Paulo anatofautisha shauku la Mkristo la mbinguni na mtu wa dunia apendaye mambo ya ulimwengu (mistari 20,21).
   1. Wenyeji wa Mkristo ni mbinguni na hapaswi kuzingatia vitu vya duniani (linga. Kol.3:1-3).
   2. Mkristo anatazamia kuja kwake Kristo na ufufuo na kubadilishwa kwa mwili huu kabla ya kwenda mbinguni (linga. 1 Kor.15:51-53).

**HITIMISHO**:
1. Paulo alifundisha katika mistari hii hitaji la kujitoa sadaka ili kuwa pamoja na Kristo.
2. Hakuna jambo lolote ambalo mtu anaweza kutoa linalolingana na furaha ipatikanayo katika Bwana, ambamo tunazidi kufurahi tunapochuchumilia lengo letu la mbinguni.

## SURA YA NNE

**UTANGULIZI**:
1. Sura hii ya mwisho ya Wafilipi imejaa maonyo (exhortations).
2. Ndugu wamehamasishwa kuwa imara katika Bwana, kuwa katika maelewano, kufurahia, na kutafakari mambo yaliyo sahihi.
3. Paulo anabainisha shukrani zake kwa zawadi zao kwake, na kuhitimisha kwa salaam kutoka kwa watakatifu, na kama kawaida yake akiwatakia baraka (benediction).

**MAZUNGUMZO**:

I. Maonyo mbalimbali yametolewa kwa kanisa na kwa mtu mmoja mmoja katika mistari 1-9.

A. Ndugu wamehamasishwa "kusimama imara katika Bwana" (mstari 1).

1. "Basi" (therefore) hurejea katika sura iliyotangulia, ambapo Paulo alijadili umuhimu wa kuenenda kwa kufuata ile sheria moja.

2. Filp.3:20,21 panapaswa kuangaliwa na 4:1.
   a. Tunapaswa kusimama imara katika Bwana kwa sababu wenyeji wetu kama Wakristo ni mbinguni.
   b. Tunapaswa kusimama imara katika Bwana kwa sababu tunajua kwamba Bwana atarudi tena na mwili wetu huu wa unyonge utageuzwa ili tupate kuwa naye milele.

3. Paulo anawataja Wafilipi kama "furaha na taji."
   a. Hapa anarejea wakati ambapo angewaona wamekubaliwa na Mungu pamoja na Kristo katika hukumu.
   b. Mbinguni tutafahamiana (linga. 1 Thes.2:19,20).

B. Mtu mmoja mmoja ameamuriwa kukaa kwa amani (4:2,3).

1. Mistari hii ina ombi juu ya akina dada wawili ili wamalize ugomvi wao, wanie mamoja katika Bwana.

2. Ni dhahiri Euodia na Sintike walikuwa na mambo fulani ya kutoelewa baina yao.

3. Paulo aliwaomba kuwa "wanie mamoja katika Bwana."
   a. Filp.2:2.
   b. Rum.12:16.
   c. Rum.15:5.
   d. 2 Kor.13:11.

4. Paulo anamtaka "mjoli wa kweli," pengine mhubiri wa kusanyiko katika Filipi, kuwasaidia akina dada hao kutatua tofauti zao.

5. Anawazungumzia watenda kazi wengine ambao majina yao "yamo katika kitabu cha uzima."
   a. Ufu.20:12.
   b. Tunaweza kujua kwamba majina yetu yameandikwa humo (linga. 1 Yoh.2:3; 5:13).

C. Mistari 4-7 ina maonyo kuhusu furaha (joyfulness) na upole (gentleness).

1. "Katika Bwana" tunaweza daima kufurahia (mstari 4).
   a. Paulo amerudia-rudia maonyo haya katika kitabu kizima.
   b. Filp.2:18; 3:1.

2. "Upole" ni kuchukuliana katika mahusiano na wengine; utu wema ndio unaolengwa katika neno hili.

3. Katika mstari 5, msemo "Bwana yu karibu" inamaanisha Bwana yu karibu kusaidia, daima akiangalia matendo na mwelekeo wetu.
   a. Hili ni wazo makini, bali lenye furaha kwa Mkristo anayetenda mapenzi ya Mungu.
   b. Ebr.4:13.

c. Katika Wafilipi 4:5, Paulo alikuwa hafundishi kwamba Yesu yu karibu kurudi, ingawa baadhi ya watu walishindwa kuelewa dhana hiyo katika kipindi cha Agano Jipya (linga. 1 Thes.4:13-18).

4. Maonyo yametolewa juu ya kujisumbua (anxiety) katika mstari 6, na kuwasihi kuomba pamoja na kushukuru.
    a. Hili hapa linamkumbusha mtu juu ya Hotuba ya Mlimani – Math.6:25.
    b. Sala husaidia kuondoa hofu.

5. Sala huleta amani itokayo kwa Mungu ambayo hutawala mioyo na nia zetu kupitia Yesu Kristo (mstari 7).
    a. Efe.6:18.
    b. Yak.5:16.

D. Katika mistari 8 na 9 Paulo anawasihi Wafilipi kutafakari na kutenda kwa haki.

1. Ni muhimu sana kwamba Mkristo kuzingatia akilini mwake mambo ambayo yametajwa katika mstari 8.
    a. Mambo yote yaliyo ya kweli.
    b. Yo yote yaliyo ya staha.
    c. Yo yote yaliyo ya haki.
    d. Yo yote yaliyo safi.
    e. Yo yote yenye kupendeza.
    f. Yo yote yenye sifa njema.
2. Ni mambo gani yanayohusisha maneno haya?
    a. Ukweli hutangulia kasha hujieleza wenyewe.
    b. Mambo yaliyo ya staha ni utu na heshima.
    c. Haki ni kutokuwa na hali yoyote ya upendeleo.
    d. Usafi unahusisha bila doa (chastity) na kuitawala nafsi.
    e. Yenye kupendeza wala si ukatili na kutafuta makosa ya wengine.
    f. Yo yote yenye sifa njema ni kujitahidi kuwa na jina jema na kutambua umuhimu wa kuwa nalo.

3. Katika mstari 9 Paulo anataka ndugu kuyatendea kazi mambo ambayo walikuwa nayo.
    a. Waliyojifunza,
    b. Waliyoyapokea,
    c. Waliyoyasikia, na
    d. Waliyoyaona.

II. Paulo anaelezea shukrani kutokana na zawadi zao za upendo (4:10-20).

A. Wafilipi walikuwa wamemsaidia Paulo hapo nyuma, walakini hawakupata nafasi wakati huu, inaonekana kuwa hawakutuma misaada kwake (mstari 10) kwa kipindi fulani.

B. Paulo anaeleza kuwa alikuwa haombi msaada kama mtu mwenye mahitaji, kwa sababu alijifunza kuishi kulingana na mazingira aliyokuwemo (mistari 11-13).
1. Paulo alijifunza:
    a. Jinsi gani ya kutokuwa na vitu,
    b. Jinsi gani ya kuwa navyo vingi na wala asijivune,
    c. Ni jinsi gani ya kushiba, akiwa amelishwa bara bara, na
    d. Jinsi gani ya kushinda na njaa.

2. Kuridhika kwa Mkristo ni somo ambalo tunapaswa kujifunza.
3. Ni nini ufunguo wa kuridhika?
    a. Kristo ndilo jibu.
    b. Alitoa kila kitu tunachohitaji ili mambo yote tuyafanye (mstari 13).

C. Mistari 14-16 sifa anazozitoa Paulo kwa ukarimu wa Wafilipi.
    1. Walituma misaada zaidi ya mara moja kwa Paulo.
    2. 2 Kor.8:1-4 Huonyesha ukarimu (liberality) wa ndugu hao.
    3. Ukarimu (generosity) ni baraka kwa mtoaji kadhalika kwake anayepokea.

D. Paulo aliwataka watoe, na wala si kwa ajili yake mwenyewe, bali wapate nguvu na kujiimarisha wenyewe (mstari 17).
    1. Wangenufaika kwa kuwasaidia wengine.
    2. Hiyo ni hazina yao mbinguni (Math.6:19,20).

E. Katika mstari 18 Paulo analinganisha zawadi zao kuwa ni sadaka iliyokubalika na Mungu.
    1. Ebr.13:16.
    2. 2 Kor.9:12.

F. Paulo anawahakikishia kwamba Mungu atawatimizia mahitaji yao, na akitoa maelezo yenye sifa nyingi mbele za Baba (mistari 19,20).
    1. Hatupaswi kujisumbua (hofu) juu ya mahitaji ya mwili.
    2. Math.6:33.
    3. Hapa haina maana tusifanye kazi, bali tujishughulishe na kuacha kuwa na wasiwasi.

G. Salaam za mwisho za Paulo na dua yake zimetolewa katika mistari 21-23.
    1. Anatuma salaam kutoka kwa ndugu kutoka Rumi (mstari 21).
    2. Miongoni mwa ndugu ni wale walioongolewa katika nyumba ya Kaisari (mstari 22).
    3. Anahitimisha kwa kuelezea shauku lake kwamba neema, au huruma wasiyostahili Wafilipi, iwe juu yao kutoka kwa Mungu Wafilipi (mstari 23).

**MWISHO:**

1. Hivyo ndivyo Paulo anahitimisha “barua yake ya upendo” kwa Wafilipi.
2. Kutokana na barua hiyo tunaweza kujifunza “nia ya Kristo,” ufunguo katika maisha yenye mafanikio kwa Mkristo na urithi wa milele.